

Ofisi ya IUCN (muungano wa uhifadhi duniani) ya afrika mashariki na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS(shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendelevu wa chuma riziki. Uchapelejia [http://www.iucn.org/water/governance/take](#) tawi wa uvuvi [http://www.cordio.no](#) Cutoka kwa mgawanyo wa kila mwaka ziongezwe. Twaomba wizara kutia mkazo uhusiano kati ya upunguzaji wa umaskini na utawala na

Kujenga Uwezo wa Jamii Kusimamia Rasilimali ya Baharini Kenya



Utangulizi

Ilani ya kisheria nambari 402 ya sheria ya uvuvi (sura 378) ina taratibu

ya uvuvi (usimamizi tawala wa vitengo vya ufukwe-BMUs) 2007.

Taratibu hizo zimeandaa njia ya kuzatiti BMU kwa kila bandari ya uvuvi katika pwani.

Shabaha za BMU miongoni mwa nyingine:

- Anzisha maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi.
- Saidia kupunguza umaskini na kuboresha ustawi na chuma riziki kwa wanachama kwa njia ya utawala bora na demokrasia, mpango wa usimamizi bora wa rasilimali na kujitegemea.
- Imarisha usimamizi wa bandari za samaki, rasilimali na kujitegemea.
- Tambua majukumu ya wadau mbalimbali wa sekta ya uvuvi, wakiwemo wanawake.
- Zua au punguano migongano ndani ya sekta ya uvuvi.

Utawala wa BMU huwa na muundo ufuatao. Kongamano la wanachama, kamati ya utendaji na kamati ndogo ndogo. Uanachama wa BMU uko wazi kwa mtu ye yeyote anaetegemea uvuvi na ufukwe kwa mapato ya kifedha au kujikimu maisha. BMU inaruhusiwa kutunga sheria zake ndogo ndogo.



Đ !

I m

JINA LA BMU	LENGO NA SHUGHULI	MASWALA NYETI
Takaungu Kilif	<ul style="list-style-type: none">• Kuwaleta pamoja wadau wote wa Takaungu• Uvuvi endelevu• Uhifadhi wa mazingira k.m upanzi wa mikoko	<ul style="list-style-type: none">• Uchafuzi wa taka kutoka kiwanda cha mkonge cha Vipingo• Ukosefu wa vifaa na ujuzi wa uvuvi• Umiliki haramu wa bandari za uvuvi na mabepari waendelezaji binafsi
Gongoni Malindi	<ul style="list-style-type: none">• Uregeshaji hali bora ya mikoko	<ul style="list-style-type: none">• Ukokooro kwenye ghuba ya Ungwana• Uharibifu wa mikoko kutoka kwa mashamba ya chumvi
Ozi Mto Tana	<ul style="list-style-type: none">• Uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili• Kupunguza umasikini	<ul style="list-style-type: none">• Ukandamizaji wa wavuvi wadogo wadogo na wafanyakishara kubwa wa samaki• Idara ya uvuvi kutowajibika kudhibiti sheria ya uvuvi.
Mida Malindi	<ul style="list-style-type: none">• Usafshaji wa ufuko• Uregeshaji wa mikoko• Kuwabandika kasa vibandiko	<ul style="list-style-type: none">• Uchafuzi wa kutoka kwa taka za matibabu• Mgongano kati ya watumiaji Wa rasilimali ya bahari(km kati ya wavuvi na wenye mashua, kati ya wavuvi, wenye hoteli na KWS)
Bamburi Mombasa	<ul style="list-style-type: none">• Hamasisha juu ya uhifadhi• Kujifunza na kuiga mbinu za kisasa za uvuvi• Kupanua matumizi mbali mbali ya rasilimali ili kuzidisha mapato ya fedha.	<ul style="list-style-type: none">• Ukosefu wa vifaa bora vya uvuvi• Ukosefu wa kituo cha mafunzo cha kuelimisha na kuhamasisha wanachama
Amu Lamu	<ul style="list-style-type: none">• Uvuvi endelevu	<ul style="list-style-type: none">• Ukosefu wa zana bora za uvuvi